



**TANZANIA PLANT HEALTH AND PESTICIDES  
AUTHORITY (TPHPA)**



**RIPOTI KUHUSU KUTOKEA KWA UGONJWA WA MAHINDI LETHAL  
NECROSIS NA VIRUSI VYAKE SHAMBANI NA KWENYE MBEGU ZA  
MAHINDI NCHINI TANZANIA**

**TAREHE: 28 Machi, 2024**

Mahindi ni chanzo muhimu cha chakula na kipato kwa wakazi wa vijijini na mijini nchini Tanzania. Uzalishaji wa mahindi barani Afrika unaweza kuathiriwa na Ugonjwa wa mnyauko wa mahindi "*Maize Lethal Necrosis Disease*" (MLND). Kufuatia ripoti ya kwanza ya kutokea kwa MLND nchini Tanzania, Wizara ya Kilimo kupitia Mamlaka yake ya Afya ya Mimea na Viuatilifu (TPHPA) kwa mujibu wa Sheria ya Afya ya Mimea Na.4 ya mwaka 2020 ilifanya tafiti za ufuatiliaji kuanzia mwaka 2016 hadi 2021 na hivi karibuni mwaka 2023 kwa lengo la kubaini maeneo yaliyoathirika katika mashamba ya mahindi na shehena za nafaka zinazosafirishwa kwenda nje ya nchi.

Utafiti wa kina wa MLND ulifanyika Kanda ya Ziwa (Mwanza, Kagera, Shinyanga, Mara), Kanda ya Kaskazini (Kilimanjaro, Manyara, Arusha) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini (Ruvuma, Njombe, Iringa, Rukwa na Katavi), Kanda ya Kati (Dodoma na Singida), Kanda ya Magharibi (Tabora) na Kanda ya Mashariki (Tanga na Morogoro). Ugonjwa wa MLND wa mahindi (*Zea mays* L.) husababishwa na mchanganyiko wa kirusi aina ya "*Maize chlorotic mottle virus*" (MCMV) na virusi vyovyote vya nafaka katika kundi la 'Potyviridae' ikiwa ni pamoja na "*Sugarcane mosaic virus*" (SCMV), "*Maize dwarf mosaic virus*" (MDMV), "*Maize mosaic virus*" (MMV) na "*Wheat streak mosaic virus*" (WSMV). Mbinu ya RT-PCR ilitumika kugundua virusi hivi kwenye sampuli zilizokusanywa mashambani na kutoka kwenye sampuli za mbegu za mahindi zilizokusanywa kutoka Mpaka wa Kasumulo mnamo Desemba 2023. Uchambuzi wa kimaabara wa sampuli hizo haukugundua virusi vyovyote kutoka kwenye nafaka za mahindi na sampuli za mashambani kutoka mikoa inayozalisha mahindi kwa wingi nchini Tanzania. Matokeo haya yanaonesha kuwa mbegu za nafaka za mahindi kutoka Tanzania hazina vihatarishi vya kusambaa kwa virusi vinavyosababisha MLND ndani na nje ya nchi. Ripoti ya kina inaweza kupatikana kwenye tovuti za Serikali ya Tanzania.

**Prof. Joseph Canisius Ndunguru**

**DIRECTOR GENERAL**